



## TAARIFA KWA UMMA

### UKUSANYAJI KODI KWENYE MICHEZO YA KUBAHATISHA

**09/08/2017**

Kupitia Sheria ya Fedha Na. 4 ya mwaka 2017, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Na:166 kwa kuipa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jukumu la kukadiria, kukusanya na kuhasibu kodi kwenye michezo ya kubahatisha kuanzia tarehe 1 Julai, 2017.

Ili kuweza kutekeleza mabadiliko hayo, Wadau wote pamoja na Walipakodi waliokuwa wakilipa kodi zao kwenye Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (Gaming Board of Tanzania) wanaelekezwa kwamba kuanzia sasa wanawajibika kuwasilisha ritani zao pamoja na kulipa kodi stahiki kwa Kamishna wa Kodi za Ndani, TRA. Ieleweke kuwa malipo ya kodi kwenye michezo ya kubahatisha yanakidhi wajibu wa Kodi ya Mapato kwa mwendeshaji wa mchezo huo katika kipindi husika.

Wadau/Walipakodi wanaelekezwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- i. Kulipa kodi inayotozwa kwenye michezo ya kubahatisha kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Na. 166;
- ii. Kusajili biashara ili kupatiwa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kwa wale wasiokuwa na usajili;
- iii. Kuwasilisha ritani za kodi ya michezo ya kubahatisha kwenye Ofisi ya TRA walikopatia usajili wa TIN.
  - ❖ Kwa wale wanaofanya biashara ya michezo ya kubahatisha katika Mkoa wa Dar es Salaam na ambao walipata Namba za Utambulisho wa Mlipakodi kwenye Mikoa ya Ki-Kodi ya Ilala, Kinondoni na Temeke watawasilisha ritani zao za michezo ya kubahatisha kwenye Ofisi ya TRA iliyopo ghorofa ya tatu, "Summit Tower" Mtaa wa Lumumba, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam. Waendesha michezo ya kubahatisha wanaofanya biashara hiyo mikoa mingine (nje ya Dar es Salaam) watahudumiwa na Mikoa ya Kodi walikopatia Namba za Utambulisho wa Mlipakodi.
- iv. Kutumia namba za utambulisho wa malipo ("**GFS Codes**") zilizoainishwa kwenye Jedwali lifuatalo pindi wafanyapo malipo husika:

**NAMBA ZA UTAMBULISHO WA MALIPO (“GFS CODE”) YA MICHEZO YA  
KUBAHATISHA KWENYE HUDUMA MAHUSUSI**

<b>Sura</b>	<b>Sura Ndogo</b>	<b>Kipengele</b>	<b>Kipengele Kidogo</b>	<b>Maelezo</b>	<b>Namba za Utambulisho wa Malipo (GFS Code)</b>
1	1	440	107	Tax on Sports Betting on stakes (sales)	11440107
1	1	440	108	Tax on Sports Betting on winnings	11440108
1	1	440	109	Tax on Slots (Route) Operation	11440109
1	1	440	110	Tax on SMS Lotteries	11440110
1	1	440	111	Tax on National Lotteries	11440111
1	1	440	112	Tax on Casino Gross Gaming Revenue (GGR)	11440112
1	1	440	113	Tax on Casino winnings	11440113
1	1	440	114	Tax on Forty Machines Site	11440114

**Wito**

Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kutoa wito kwa Walipakodi wote ikiwa ni pamoja na Waendesha michezo ya kubahatisha kuwasilisha ritani na kulipa kodi stahiki ndani ya muda uliowekwa kisheria ili kuchangia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Taifa na kuepuka adhabu na gharama zisizo za lazima zitokanazo na kutokulipa kodi kwa wakati.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali usisite kuwasiliana na kituo cha huduma kwa walipakodi kwa kupiga simu za bure: 0800750075/0800780078, Barua pepe [huduma@tra.go.tz](mailto:huduma@tra.go.tz)**

***“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”***

**Imetolewa na Kamishna wa Kodi za Ndani-Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**